

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Mtaa wa Mahakama,
S. L. P. 1419,
53103 MBEYA.
Simu: (025) 252503566
Nukushi: (025) 252502958
Barua pepe: rbcmbeya@pccb.go.tz
Wavuti: <http://www.pccb.go.tz>

TAARIFA KWA UMMA

MBEYA – AGOSTI 20, 2020

**AFIKISHWA MAHAKAMANI NA TAKUKURU
KWA KUSHAWISHI NA KUTOA RUSHWA**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Mbarali Mkoani Mbeya leo tarehe 20/08/2020 imefungua shauri la jinai Na. 153/2020 katika Mahakama ya Wilaya ya Mbarali dhidi ya Bw. Lea Nkani Magembe (Mkulima). Mshitakiwa anashitakiwa kwa kosa la kushawishi na kutoa rushwa ya sh. 800,000/= kwa Afisa Mtendaji wa Kata ya Itambuleo Bw. Rashidi Ngovano ili amsaidie kumuachisha shule mtoto wake aitwaye Rambo Lea Nkani anayesoma kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Itambuleo ili akaolewe kwa madai kuwa mtoto wake ni mkubwa na anahofia akienda shule atapata mimba kosa ambalo ni kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007.

Tukio hili limetokea baada ya Afisa Mtendaji wa kata hiyo kuendesha zoezi la kuwakamata wazazi ambao watoto wao hawajarejea shule baada ya tatizo la Corona.

Mshtakiwa huyo amekiri kosa na kupewa adhabu ya kulipa faini ya sh. 600,000/= au kifungu cha miaka mitatu. Mtuhumiwa amelipa faini. Pamoja na adhabu hiyo Mahakama imetaifisha fedha za rushwa kiasi cha kiasi cha sh. 800,000/= alizokuwa ametoa kuwa mali ya Serikali.

WITO KWA WANANCHI

Tunawapongeza wananchi wa Wilaya ya Mbarali na mkoa wa Mbeya kwa ujumla kwa kuendelea kushirikiana na Taasisi yetu katika mapambano dhidi ya rushwa. Tunaahidi kuzifanyia kazi taarifa zenu kwa haraka na kwa weledi wa hali ya juu. Nawaomba muendeleo kutumia Huduma ya simu ya dharura kwa kupiga namba 113, kuandika ujumbe mfupi wa maneno kwenda namba 113 au kubonyeza *113# na kufuata maelekezo. Huduma hii ni BURE na ni rahisi kwa mtu yeyote mwenye simu ya mkononi kuitumia.

IMETOLEWA NA:

**JULIETH MATECHI
MKUU WA TAKUKURU MKOA WA MBEYA**
